



TAARIFA KWA UMMA

MWALIKO WA MKUTANO WA WADAU KUPOKEA MAONI KUHUSU MAREJEYO YA NAULI ZA MABASI YA MASAFYA MAREFU NA MABASI YA MIJINI (DALADALA), JUMATANO, 18 OKTOBA, 2023, DAR ES SALAAM

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imepokea maombi kutoka kampuni tatu (3) zinazotoa huduma ya usafiri wa abiria wa masafa marefu; **Super Feo Enterprises, ABC Upper Class and Transportation Ltd** na **Happy Nation Co. Ltd**, wakiiomba Mamlaka kufanya marejeo ya nauli za mabasi kutohana na ongezeko la gharama za uendeshaji, ikiwemo kupanda kwa bei ya mafuta (petroli na diseli). Mapendekezo ya kampuni hizo ni kuongeza **nauli ya sasa ya Shilingi 56.88 kwa Kilometra 1 kwa kila abiria** kama ifuatavyo:

Na.	Kampuni	Aina ya Huduma	Nauli Pendekewza kwa Kilometra 1 kwa kila abiria	Ongezeko kwa Kilometra 1 kwa kila abiria	
			Shilingi	Shilingi	%
1.	Super Feo Enterprises	Daraja la Kati	101.88	45.00	79.11
2.	ABC Upper Class and Transportation Ltd	Daraja la Kati	92.84	36.96	63.22
3.	Happy Nation Co. Ltd	Daraja la Kati	84.06	27.18	47.78

Kwa kuzingatia kifungu cha 21 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Sura ya 413 pamoja na kanuni ya 9(3) ya Kanuni za LATRA (Tozo) za Mwaka 2020 (Tangazo la Serikali Na. 82 la tarehe 7/2/2020), Mamlaka inapaswa kutoa fursa kwa kampuni hizi kuwasilisha mapendekezo yao kwa wadau wa usafiri wa abiria kisha kukusanya maoni ya wadau kabla ya kufikia uamuzi wa kufanya marejeo ya nauli zilizotumika. Nauli zinazotumika kwa sasa zilitangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 18 la tarehe 6 Mei, 2022.

Hivyo, Mamlaka imeandaa mkutano wa wadau kupokea maoni juu ya mapendekezo ya watoa huduma ya kufanya marejeo ya nauli za mabasi ya masafa marefu. **Mkutano huo**

utafanyika Dar es Salaam, siku ya Jumatano, tarehe 18 Oktoba, 2023, katika ukumbi wa Arnaoutougloou kuanzia saa 3:00 asubuhi.

Aidha, katika Mkutano huu, **LATRA itawasilisha mapendekezo ya vigezo vya mchakato wa kuridhia mapitio ya viwango vya nauli za mabasi yanayotoa huduma mijini (daladala).** `Wasilisho la LATRA litafanywa kwa mujibu wa kanuni ya 13 ya Kanuni za LATRA (Tozo) za Mwaka 2020 (Tangazo la Serikali. Na. 82 la tarehe 7/2/2020),

Kutokana na umuhimu wa suala hili, LATRA inawaalika wadau wote wa usafiri wa umma na Wananchi kwa ujumla kuhudhuria mkutano huu muhimu ili kutoa maoni baada ya kusikiliza mapendekezo yatakayowasiliishwa na kampuni zilizoleta maombi ya kufanya marejeo ya nauli za mabasi ya masafa marefu, pamoja na wasilisho la LATRA kuhusu nauli za mabasi ya mijini (daladala). Mamlaka inawasihi wamiliki, watoa huduma na Wananchi wote kwa ujumla kushiriki ipasavyo katika zoezi hili ili liweze kukamilika mapema.

ANGALIZO:

Wakati mchakato huu ukiendelea, Mamlaka inawashauri wamiliki wa mabasi na watoa huduma wote wa usafiri wa umma kuendelea kuzingatia masharti ya leseni zao kwa kutojipangia nauli kinyume na Sheria. **Adhabu ya kutoza nauli isiyo halali ni Shilingi 250,000/- kwa mujibu wa kanuni ya 30 ya Kanuni za Leseni za Usafirishaji (Mabasi ya Abiria) za Mwaka 2020 (Tangazo la Serikali Na. 76 la tarehe 7/2/2020).** Mamlaka haitasita kuchukua hatua stahiki kwa mmiliki au mtoa huduma ye yeyote atakayekiuka Sheria na Masharti ya Leseni yake.

Imetolewa na:

Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano – LATRA

12 Oktoba, 2023